OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

MKUU WA SHULE 0719407373
MAKAMU MKUU WA SHULE 0718100398
PATRON .0752017239

MSAMALA SEKONDARI,
S. L. P. 599,
SONGEA.
30/03/2022

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHUL E YA SEKONDARI MSAMALA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEAA, MKOA WA RUVUMA MWAKA 2022/2023

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa Mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari Msamala mwaka 2022/2023 tahasusi ya.....

Shule ya Sekondari Msamala ipo umbali wa kilometa sita (6) kaskazini mwa mji wa Songea. Kwa wageni kabisa shuka gari kituo kikuu cha mabasi kilichopo SHULE YA TANGA, Panda Daladala kuelekea mjini na shuka kituo kiitwacho MTAZAMO, Hapo zinapatikana pikipiki kwa shilingi 1,000/= mpaka Shule ya Sekondari Msamala.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 05/09/2022 hivyo, Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 05/09/2022 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/09/2022

2. Mambo muhimu ya kuzingatia;

2.1. Sare ya Shule

i. Sare ya shule ni rangi ya Esteem namba 9 ambayo imebandikwa juu ya fomu hii, na mshono wa suruali uwe wenye marinda matatu, pamoja na upana wa size 16 chini, pamoja na tai yenye rangi ya suruali ikiwa na alama "V" (alama "V" iwe ya rangi ya kijani)
ii. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu liwe pana, lisiwe la kubana.
iii. Sare ya michezo ya shule hii ni "Track suit" ya bluu pia aje na bukta ya michezo pamoja na fulana yake rangi yoyote.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
v. Soksi jozi mbili nyeusi.
vi. Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
vii. Sweta angalau 1 rangi ya bluu yenye shingo la V mbele.
viii. T-shirt ya "Dark blue" 1 yenye nembo ya shule (zinapatikana shuleni kwa sh. 10,000/=)
ix. Suruali ya kushindia rangi ya "Dark blue".

NB: Nguo nyingine ambazo ni nje ya maagizo haziruhusiwi kabisa. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayekutwa nazo. Pia, tunashauri mwanafunzi afike kushona suruali, tai na T-shirt kununua shuleni baada ya kusajiliwa ili kuepuka mkanganyiko wa rangi na mitindo ya ushonaji kwa gharama zifuatazo;-

- Suruali ya shule kwa shilingi 20,000/=
- Suruali ya kushindia kwa shilingi 20,000/=
- Tai shilingi 2,000/=
- T-shirt ya dark blue kwa shilingi 10,000/=

Fedha hizi zote zilipwe kwenye akaunti namba 61803500056 NMB. Jina la akaunti ni Msamara Sekondari. Tafadhali usiingize kwenye akaunti tofauti na hii kwani utachelewa kupata sare kwa wakati.

2.2 Ada na michango ya shule;

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= unaweza kulipa shilingi 35,000 kwa muhula ua kulipa yote kwa mara moja.
(b) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
(c) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma alipe shilingi 10,000/= kwa muhula
(d) Shilingi 35,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine. (Alipe shilingi 15,000/= kwa muhula wa kwanza na 20,000/= muhula wa pili.
(e) Fedha ya tahadhari shilingi 5,000/= (haitarejeshwa)
(f) Shilingi 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule
(g) Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza
(h) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
(i) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima.

Jumla ya michango na ada kwa mwanafunzi ni shilingi 188,000/= kwa mwaka. Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule namba 61801200088 katika benki ya NMB. Jina la akaunti ni Msamala Sekondari.

NB: Kwa asiye na bima ya afya, mzazi unashauriwa kumlipia mwanao shilingi 50,400/= kwa ajili ya bima ya afya kwa mwaka mmoja. Pesa hiyo ilipwe yote kwa mara moja. Na fedha hiyo ilipwe kwenye akaunti namba 61803500056 NMB ya Msamara Sekondari.

2.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni;

i) Ream ya karatasi nyeupe 1
ii) Graph pad 1
iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
v) Scientific calculator (isipokuwa kwa wanafunzi wa tahasusi ya HKL, HGK, na HGL)
vi) Godoro 1
vii) Mashuka pair 2 ya rangi ya blue bahari, blanket 1, foronya 1, chandarua 1.
viii) Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
ix) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
x) Soft broom 1, hard broom 1, drier 1, jembe 1, fyekeo 1 na fagio ya chelewa 1

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
vi) Kufuga nywele na ndevu.
vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
viii) Uvutaji wa sigara
ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xi) Kusababisha mimba
xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiv) Kudharau bendera ya Taifa.
xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Pamoja na maelekezo hayo tumeambatisha na;**

(a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5. Mwanafunzi aje na picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea shuleni pamoja na namba zao za simu.

6. Aje na nakala ya result slip kwa ajili usajili pamoja na jalada (file) la kutunzia nyaraka hizo.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na uyatekeleze kwa ukamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

.....

Godfrey Ponera
MKUU WA SHULE

HEADMASTER
MSAMALA SECONDARY SCHOOL
Box 599-SONGEA

KIAMBATISHO A
MEDICAL EXAMINATION FORM

SONGEA MUNICIPAL COUNCIL

MSAMALA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 599,
SONGEA

30/03/2022

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine Mr..... as to his physical and mental fitness for admission as a form FIVE student for the Academic year 2022/2023

Yours sincerely,

.....
THE HEADMASTER

HEADMASTER
MSAMALA SECONDARY SCHOOL
Box 599-SONGEA

The Headmistress, I have examined Mr/Miss..... as shown below and consider that he is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full time secondary school education.

1. Vision with/without glasses. Right .....
   Left.....
2. Blood pressure.....
   Hemoglobin.....
3. Hearing.....
4. (a) Urine Albumen.....
   (b) Sugar.....
5. (a) venereal diseases..... ....
   (b) Bilharzias.....
6. Pregnancy.....
7. Neurosis.....
8. Is there any abnormality of:-
   (a) The heart..... (b) Lungs.....
   (c) The spleen.....
9. Are there any serious disease e.g. leprosy, asthma, diabetes, etc

.....

Date: .....
Station: .....

.....
Signature of Medical Officer
Designation.....

KIAMBATISHO C

AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU

□ Mimi ..... nakubali nafasi niliyopata katika shule ya sekondari ya Msamala kuendelea na masomo.

□ Nafahamu kuwa ninagharamiwa na Taifa linalothamini kazi na juhudi

□ Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa upeo na uwezo wangu kuwa mwanafunzi mwema.

□ Ninaahidi kutoshiriki katika mambo yatakayosababisha mwanafunzi kuachishwa shule.

□ Naahidi kuwa nitashirikiana na walimu pamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa shule na Taifa kwa ujumla.

.....

Saini ya Mwanafunzi

Mimi.....

Mzazi wa ..... nimesoma maelekezo yote na kuelewa. Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua. Ripoti na barua zote zinazohusu mtoto wangu ziletwe kwangu kwa anuani:-

.....

.....

.....

Jina la mzazi.....Mtaa..... Saini ya mzazi..... Balozi.....

Tarehe..... Namba yaSimu.....

KIAMBATISHO B

KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi.....
2. Tarehe ya kuzaliwa..... Mahali.....
3. Jina la baba/Mlezi.....hai/amefariki.....
4. Mahali anakoishi:Kijiji/Mji.....Wilaya.....Mkoa.....
5. Kazi ya baba/Mlezi.....
6. Namba yake ya simu.....
7. Jina la mama/mlezi.....
8. Mahali anakoishi:Kijiji/Mji.....Wilaya.....Mkoa.....
9. Kazi ya Mama/Mlezi.....
10. Namba yake ya simu.....

NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

NA	JINA	UHUSIANO	NAMBA YA SIMU